



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**



TANGAZO LA MABADILIKO YA TAREHE YA KUENZA MINADA

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inawatangazia wadau wote wa tasnia ya korosho kuwa kutokana na changamoto za kimtandao, zilizosababisha baadhi ya maghala kushindwa kupokea mizigo ya korosho, minada iliyokuwa inatarajiwa kuanza tarehe 31 Oktoba, 2025 imesogezwa mbele, ambapo sasa minada hiyo itaanza tarehe 7 Novemba 2025.

Aidha ifahamike kwamba shughuli zote za mauzo ya korosho kuanzia upokeaji mizigo ghalani, vibali vya kusafirisha korosho pamoja na minada yenyewe huhitaji mtandao ili kuweza kufanyika, kwa kutambua kwamba kuanzia msimu uliopita tumekuwa tukitumia mfumo wa Soko la Bidhaa (TMX) kuuza korosho kwa njia ya mtandao, jambo ambalo limekuwa na ufanisi mkubwa katika kuongeza ushindani katika minada. Lengo la kusogeza minada mbele kwa muda wa wiki moja, ni kuwezesha mizigo ya wakulima kupokelewa ghalani na kuwawezesha wanunuzi kushiriki kikamilifu katika minada kutoka popote walipo duniani.

Hivyo ili kuhakikisha kuwa wanunuzi wengi wanaweza kushiriki katika minada ni lazima kuwe na mtandao wa uhakika ikiwa ni pamoja na kurahisisha shughuli za upokeaji wa korosho ghala kuu na utoaji vibali vya usafirishaji.

Wadau wote katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho kutoka ndani na nje ya nchi wanaombwa kuwa na subira katika kipindi hiki kwani ni matarajio yetu kuwa hadi kufikia jumatatu ya tarehe 3 Novemba, 2025 hali ya mtandao itakuwa shwari na hivyo kuwezesha mizigo kupokelewa ghalani, na kuwezesha minada kuanza kufanyika tarehe 7 Novemba, 2025.

Aidha, nichukue fursa hii kuwaomba warajis wasaidizi wa Mikoa pamoja na Viongozi wa Ushirika kuendelea kuwaelimisha na kusimamia ukusanyaji wa korosho kutoka kwa wakulima na usafirishaji wa korosho hizo kutoka Vyama Vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) kwenda ghala kuu. Pia, niwaombe Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za ghala kusimamia upokeaji wa mizigo ghalani, pamoja na kuandaa utaratibu wa kupokea korosho ambazo tayari magari yamefika ghalani, ili kuendana na mabadiliko haya yaliyotokea.

Mwisho niwaombe radhi wadau wote kwa usumbufu utakaojitokeza kutokana na mabadiliko haya yaliyosababishwa na changamoto ya mtandao.

Usikiapo tangazo hili mtaarifu na mwingine.

Tangazo hili Limetolewa na:

MKURUGENZI MKUU

BODI YA KOROSHO TANZANIA

30 OKTOBA 2025